# MUWALA WA VIPENGELE VYA FANI: UHAKIKI WA KAZI ZA S.A.MOHAMED

NA

MUTUKU KAVOI

Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza
baadhi ya mahitaji ya shahada ya
"Master of Arts" katika:

Idara ya Lugha na Isimu,

Chuo Kikuu cha Egerton.

Novemba 1996.

X

EULIB

021 049

YALIYOMO

UNGAMO........................................ ii
HIFADHI ZA UCHAPISHAJI................... iii
TABARUKU..................................... iv
SHUKRANI .................................... v
YALIYOMO .................................... vii
MUHTASARI ................................... xi

**SURA YA KWANZA**

1.1 UTANGULIZI ................................ 1
1.2 Mada ya Tasnifu ........................... 2
1.2.1Vijelezi na Fafanuzi za Dhana Mbalimbali. 5
1.3 Madhumuni ya Utafiti ...................... 9
1.4 Makisio ya Utafiti ......................... 10
1.5 Sababu za Kuchagua Mada hii ............... 10
1.6 Upeo wa Utafiti ........................... 12
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada hii ............. 14
1.8 Misingi ya Nadharia ....................... 36
1.9 Mbinu za Utafiti .......................... 43

**SURA YA PILI**

**MAISHA YA SAID AHMED MOHAMED, FANI NA VIPENGELE VYAKE, FANI NA MAUDHUI**

2.1 UTANGULIZI ................................ 46
2.2 MAISHA YA SAID AHMED MOHAMED............... 47
2.3 FANI NA VIPENGELE VYAKE.................... 51
2.3.1 PLOTI...................................... 51
2.3.1.1 VIGEZO VYA PLOTI......................... 53
2.3.1.2 AINA ZA PLOTI............................ 57
2.3.1.2.1 Ploti Msago ............................ 57
2.3.1.2.2 Ploti Kioo ............................. 58
2.3.1.2.3 Ploti Rejeshi .......................... 58
2.3.2 MUUNDO WA PLOTI ........................... 59
2.3.2.1 Maelezo ................................. 60
2.3.2.2 Mgogoro Katika Riwaya ................... 61
2.3.2.3 Upeo wa Juu ............................. 62
2.3.2.4 Suluhisho ............................... 63
2.3.3 **WAHUSIKA NA UHUSIKA**.............. 64
2.3.3.1 Dhana ya Wahusika ....................... 65
2.3.3.2 UFUNUZI WA WAHUSIKA...................... 67

2.3.3.2.1 Ufunuzi wa Kimaelezo .............. 68
2.3.3.2.2 Ufunuzi wa Visa vya Kimatendo ..... 70
2.3.3.2.3 Ufunuzi wa Kulinganisha na Kutofautisha Wahusika............... 71
2.3.3.2.4 Ufunuzi wa mhusika Kujipambanua au kupambanuliwa na Wengine .......... 72
2.3.3.2.5 Ufunuzi wa Kimdokezo ............. 74
2.3.3.2.6 Ufunuzi wa Kimajazi ............... 75
2.3.3.2.7 Ufunuzi wa Kiishara au Kipicha .... 77
2.3.3.2.8 Ufunuzi wa Kiploti ................ 78
2.3.3.2.9 Ufunuzi wa Kiitikadi .............. 79
2.3.3.3 UBUNAJI WA WAHUSIKA................... 80
2.3.3.4 AINA MBALIMBALI ZA WAHUSIKA........ 86
2.3.3.4.1 Wahusika kotekote(duara,mviringo).. 87
2.3.3.4.2 Wahusika Bapa...................... 88
2.3.3.4.2.1 Wahusika Bapa-sugu .............. 89
2.3.3.4.2.2 Wahusika Bapa-majazi(vielelezo).. 90
2.3.3.4.2.3 Wahusika Bapa-takriri ........... 90
2.3.3.4.3 Wahusika Vinyago au Kerekecha ... 91
2.3.3.4.4 Wahusika Shinda (Wafoili) ....... 92
2.3.3.4.5 Wahusika Jumui .................. 92
2.3.3.4.6 Wahusika Vimelea ................ 93
2.3.4 **MANDHARI**...................... 95
2.3.4.1 MAJUKUMU YA MANDHARI............. 97
2.3.4.1.1 Mandhari na Maudhui ............ 97
2.3.4.1.2 Mandhari na Wahusika............ 98
2.3.4.1.3 Mandhari na Uhalisia ........... 100
2.3.4.1.4 Mandhari na Taashira ........... 101
2.3.4.1.5 Mandhari na Hisia .............. 102
2.3.5 **MTINDO** ........................ 103
2.4 MJADALA KUHUSU USAWA WA FANI NA MAUDHUI........................... 107
2.5 HITIMISHO......................... 111


---

SURA YA TATU

FANI KATIKA DUNIA MTI MKAVU NA KIZA KATIKA NURU


3.1 UTANGULIZI............................ 114
3.2 PLOTI ................................ 114
3.2.1 PLOTI YA DUNIA MTI MKAVU............... 114
3.2.2 PLOTI YA KIZA KATIKA NURU ............ 123
3.3 **WAHUSIKA NA UHUSIKA** ................ 130

3.3.1 WAHUSIKA NA UHUSIKA
KATIKA <u>DUNIA MTI MKAVU</u>.................... 130
3.3.2 WAHUSIKA NA UHUSIKA
KATIKA <u>KIZA KATIKA NURU</u>................... 139
3.4 MANDHARI ............................ 155
3.4.1 MANDHARI KATIKA <u>DUNIA MTI MKAVU</u> .......... 155
3.4.2 MANDHARI KATIKA <u>KIZA KATIKA NURU</u> ........ 163
3.5 MTINDO............................... 167
3.5.1 MTINDO WA <u>DUNIA MTI MKAVU</u> ............... 168
3.5.2 MTINDO WA <u>KIZA KATIKA NURU</u> .............. 188
3.6 HITIMISHO ............................ 204

---

**SURA YA NNE**

**FANI NA MIKTADHA YA KIJAMII NA KIJIOGRAFIA**

4.1 UTANGULIZI.............................. 207
4.2 Miktadha ya Kijamii na Kijiografia......... 207
4.3 PLOTI NA MIKTADHA YA
KIJAMII NA KIJIOGRAFIA..................... 210
4.4 UMBAJI WA WAHUSIKA NA
MIKTADHA YA KIJAMII NA
KIJIOGRAFIA................................ 219
4.5 MANDHARI NA MIKTADHA YA KIJAMII
NA KIJIOGRAFIA............................. 234
4.6 MTINDO NA MIKTADHA YA KIJAMII
NA KIJIOGRAFIA............................. 240
4.7 HITIMISHO ............................... 248

---

**SURA YA TANO**

**MUWALA WA VIPENGELE VYA FANI**

5.1 UTANGULIZI.............................. 251
5.2 Dhana ya Muwala ......................... 252
5.3 MUWALA WA PLOTI, UUMBAJI WA WAHUSIKA,
MANDHARI NA MTINDO WA <u>DUNIA MTI MKAVU</u> ... 254
5.4 MUWALA WA PLOTI, UUMBAJI WA WAHUSIKA,
MANDHARI NA MTINDO WA <u>KIZA KATIKA NURU</u>... 268
5.5 USAWA WA FANI NA MAUDHUI ................ 279
5.6 HITIMISHO ............................... 284

---

SURA YA SITA

HITIMISHO


6.1 UTANGULIZI .......................... 286

6.2 Muhtasari wa Tasnifu .................. 286

6.3 Mahitimisho ya Tasnifu ................ 290

6.4 Matokeo ya Utafiti .................... 294

6.5 Matatizo Tuliyokumbana nayo
Katika Utafiti.......................... 298

6.6 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi........... 299

---

MAREJEO................................... 300

VIAMBATISHO

Kiambatisho cha Kwanza.................... 313

Kiambatisho cha Pili...................... 315

Kiambatisho cha Tatu...................... 316

## MUHTASARI

Tasnifu hii inajikita katika uchunguzi wa fani katika riwaya mbili za Said Ahmed Mohamed. Riwaya zenyewe ni Dunia Mti Mkavu (1980) na Kiza Katika Nuru (1988). Tunaoyesha kuwa Mohamed, kama baadhi ya watunzi wengine wa kazi za ubunifu, ameathiriwa na miktadha ya kijamii na kijiografia katika uchujaji na uchotaji wa mbinu za kifani. Aidha, tunabainisha kuwa, ili kazi ya ubunifu idhihirishe utimilifu wa kifasihi, ni sharti vipengele vya fani vionyeshe muwala au muumano. Katika mkabala huu, tumeonyesha jinsi riwaya ya Dunia Mti Mkavu ilivyokosa muwala ikilinganishwa na riwaya ya Kiza katika Nuru, hivyo umaarufu wake kutopata uhai.

Vilevile, tunaonyesha kuwa vipengele vya fani na maudhui vinachukua uzito sawa katika kazi ya kubuni--hakuna kipengele kinachojitokeza kuwa muhimu zaidi ya kingine. Ili kufanikisha maazimio yetu, tumeshughulikia vipengele vya ploti, wahusika na uhusika, mandhari na mtindo.

Tasnifu hii imegawanywa katika sura sita kuu. Sura ya kwanza, hasa, ni utangulizi. Sura hii inafafanua mada ya tasnifu yetu, madhumuni ya utafiti, umuhimu wa mada tunayoshughulikia, nadharia zinazotuongoza katika utafiti huu, upeo wake, tafiti za awali kuhusiana na mada hii pamoja na mbinu za kitafiti tunazozitumia ili kufanikisha utafiti wetu. Sura ya pili inatoa, kwa muhtasari, maisha ya Said Ahmed Mohamed ambayo ni muhimu katika sura ya nne

tunapochunguza athari za mazingira zinazomwathiri Mohamed katika uchujaji na uchotaji wa mbinu za kifani. Ni katika sura hii ambapo tumevijadili vipengele muhimu vya fani ambavyo ndivyo nguzo ya kazi ya kubuni. Kwa jumla, sura hii ndiyo msingi wa yanayofuata katika sura ya tatu.

Sura ya tatu inajihusisha na uhakiki wa vipengele vya fani katika riwaya tunazozifanyia utafiti. Sura hii ndiyo nguzo kuu, na inajenga msingi wa yale yanayojadiliwa katika sura za nne na tano. Ni katika sura hii, ambapo tumekadiria tafiti za awali kuhusiana na fani. Vipengele vya ploti, wahusika, mandhari na mtindo vimejadiliwa kwa marefu na mapana.

Sura za nne na tano ndizo kiini cha tasnifu nzima. Tunaonyesha katika sura ya nne jinsi Said Ahmed Mohamed anavyoathiriwa na miktadha ya kijamii na kijiografia. Sura ya tano inaonyesha bayana jinsi muwala wa vipengele vya fani katika riwaya ya Dunia Mti Mkavu unavyofifia, hivyo kuikosesha ukamilifu na utimilifu wa kifasihi. Pia, inaonyesha Mohamed amejenga vipengele vya fani huku vikidhihirisha muwala katika Kiza Katika Nuru, jambo ambalo linaifanya kudhihirisha utimilifu wa kifasihi. Halikadhalika, ni katika sura hii ambapo tunaonyesha usawa wa fani na maudhui baada ya kuhakiki vipengele vya fani na kuchunguza muwala wake.

Hatimaye, katika sura ya sita, ambayo ndiyo ya mwisho, tunatoa muhtasari wa tasnifu nzima na matokeo ya utafiti

wetu. Pia, sura hii inaangaza matatizo tuliyokumbana nayo katika utafiti huu. Baadhi ya mapendekezo zaidi ya utafiti, yanapatikana katika sura hii.